# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 049

JANUARI 2025

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 UZINDUZI WA MRADI WA MFUKO WA UMOJA WA MATAIFA WA KUIMARISHA UANGAZI WA HALI YA HEWA

## 2 WADAU WATAKIWA KUFUATILIA NA KUZITUMIA TAARIFA ZA HALI YA HEWA ZA TMA



## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2025



KITAIFA

# WADAU WATAKIWA KUFUATILIA NA KUZITUMIA TAARIFA ZA HALI YA HEWA ZA TMA

**Dodoma**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilikutana na wadau kutoka sekta mbalimbali nchini ili kujadili Utabiri wa Mvua za Msimu wa MASIKA 2025. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF, Dodoma tarehe 20 Januari 2025.

Akifungua mkutano huo Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakari aliwataka wadau kufuatilia na kuzitumia taarifa za hali ya hewa za TMA. kwa kuwa ni sahihi kwa asimia kubwa. “Ninawataka wadau wote nchini kufuatilia na kuzitumia ipasavyo taarifa za hali ya hewa za TMA ambazo kwa asilimia kubwa zimekuwa ni sahihi kwa mustakabali wa maslahi mapana ya Taifa letu”.

Mhe. Jaji Mshibe aliongelea kuhusu changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa ikihusisha athari mbalimbali zinazoendelea kujitokeza hapa nchini ikiwemo ukame, mvua kubwa, ongezeko la joto ambalo limeathiri shughuli za uvuvi na upatikanaji wa samaki.

Aidha, Mhe. Jaji Mshibe Ally Bakari aliiagiza TMA kuendelea na utaratibu wa kuwakutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali kupitia mikutano hiyo ikiwa ni maandalizi ya mapema kabla ya kutoa utabiri wa hali ya hewa kwa msimu husika.



Awali wakati akimkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi (IPCC), Dkt. Ladislaus Chang'a aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wa maendeleo kwa kuendelea na uwekezaji katika miundo mbinu ya hali ya hewa.

"Tunaishukuru Serikali na wadau wa maendeleo kwa kuendelea na uwekezaji katika miundombinu ya hali ya hewa hapa nchini kupitia mpango wa bajeti na programu mbalimbali za maendeleo na kuiwezesha Mamlaka kuongeza usahihi na ubora wa utabiri wa hali ya hewa.

Aidha, Dkt. Chang'a aligusia kuhusiana na ongezeko kubwa la joto duniani lililovunja rekodi kwa ongezeko la nyuzi joto 1.550c ikiwa ni ongezeko kubwa kutokea katika historia ya dunia, japo kwa hapa nchini liliongezeka kwa nyuzi joto 0.70c.



## KIMATAIFA

# UZINDUZI WA MRADI WA MFUKO WA UMOJA WA MATAIFA WA KUIMARISHA UANGAZI WA HALI YA HEWA

**Dodoma**




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) alizindua rasmi awamu ya utekelezaji wa mradi wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuimarisha Uangazi wa Hali ya Hewa (SOFF) kupitia hafla iliyofanyika mjini Dodoma.

Mpango huu mkubwa unaofanywa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Taasisi ya Hali ya Hewa ya Denmark (DMI), unalenga kuimarisha uwezo wa Tanzania wa kufanya uangazi wa hali ya hewa, ubadilishanaji wa data za hali ya hewa na katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu alisema "uzinduzi wa awamu ya utekelezaji wa mradi wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuimarisha Uangalizi wa Hali ya Hewa (SOFF) ni hatua muhimu kwa Tanzania na jumuiya za kimataifa." Aliendelea kusema, "Utaongeza uwezo wa Tanzania katika kukusanya na kusambaza data za hali ya hewa, mpango huu utasaidia kujiandaa katika kukabiliana na maafa yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa, na kuzisaidia sekta muhimu kama vile kilimo, nishati na usafirishaji katika kufanya maamuzi sahihi. Aliongeza kuwa mradi wa SOFF unaendana na mikakati ya Serikali ya kuleta maendeleo kwa ustawi na uendelevu wa Taifa.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile (MB), alisisitiza kuwa "SOFF sio tu inawekeza katika teknolojia ya kisasa bali ni kichocheo cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi sababu data sahihi za hali ya hewa huokoa na kulinda maisha na kuleta

maendeleo endelevu." Naibu Waziri alieleza kuwa Wizara ya Uchukuzi ambayo inasimamia sekta ya hali ya hewa nchini Tanzania inatambua kuwa mafanikio ya mpango wa SOFF yanategemewa kuwa endelevu na kuleta manufaa ya muda mrefu.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Shirika la Hali ya Duniani (WMO) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), Dk. Ladislaus Chang'a alisisitiza namna mradi wa SOFF unavyosaidia katika kukabiliana na mapungufu yaliyobainika katika miundombinu ya hali ya hewa nchini Tanzania ili kukidhi viwango vya Kimataifa vya Mtandao wa Kimataifa wa Uangazi wa Msingi (GBON). Utafiti wa mapungufu hayo ulifanyika mwaka 2023, "ulionyesha kuwa Tanzania inahitaji angalau vituo 27 vya uangazi usawa wa ardhi kwa eneo la kilomita 200 kwa kilomita 200, na vituo vitano (5) vya uangazi angani kwa eneo la kilomita 500 kwa kilomita 500."






Naye Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Shigeki Komatsubara, aliipongeza Serikali kwa hatua inayochukua katika kufanya mipango ya kukabiliana na maafa, akisema kuwa "SOFF itakuwa ni nyenzo muhimu ya kuwezesha mifumo ya utoaji wa tahadhari za mapema, kusaidia kufanya mifumo hii kuwa ya uhalisia kwa jamii zilizo hatarini ulimwenguni." Alisema hayo akienda sawa na mpango wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Tahadhari za Mapema kwa Wote, unaolenga kuhakikisha, ifikapo mwaka 2027, kila mtu Duniani analindwa na mifumo madhubuti ya tahadhari za mapema.



Jumla ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya uwekezaji wa mradi wa SOFF nchini ni dola milioni 13.9, ambapo dola milioni 9 zinatolewa na Mfuko wa Mashirika ya Wadau wa Hisani (Multi-Partner Trust Fund (MPTF)) huku sehemu iliyobaki ikifadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi wa SOFF ni hatua kubwa katika kuboresha miundombinu ya data za hali ya hewa kitaifa na kimataifa, kuwezesha maamuzi sahihi ya kusaidia ustahimilivu wa kiuchumi na kimazingira. Kama sehemu ya mradi huo, Tanzania itanufaika kwa kuimarisha mifumo ya uangazi, teknolojia ya kisasa, pamoja na ushirikiano wa kimataifa.

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2025 mvua za Msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuendelea hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza ya mwezi ikifuatiwa na upungufu.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa hususan wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo machache.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa, hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |

# JE WAJUA?

Unaweza kupata huduma za hali ya hewa katika maeneo mbalimbali nchini?. Tembelea ofisi zetu zilizopo nchi nzima ili kupata huduma za hali ya hewa zinazotolewa kila siku kwa muda wa saa 12 hadi 24.

## Vituo vikuu vya hali ya hewa

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 203 | 027 | 0625922118 | arusha@meteo.go.tz |
| 2 | Bukoba | 192 | 028 | 0762959909/ 0755367728 | bukoba@meteo.go.tz |
| 3 | Dodoma | 27 | 026 | 0736674360 | dodoma@meteo.go.tz |
| 4 | Handeni | 115 | 027 | 0754650633 | handeni@meteo.go.tz |
| 5 | Iringa | 114 | 026 | 0754208845 | iringa@meteo.go.tz |
| 6 | Kigoma | 278 | 028 | 0746531918/ 0737131906 | kigoma@meteo.go.tz |
| 7 | KIA | 3 | 027 | 0713339998 | kia@meteo.go.tz |
| 8 | Mahenge | 268 | 023 | 0738987638 | mahenge@meteo.go.tz |
| 9 | Songwe | 128 | 025 | 0765908951 | songwe@meteo.go.tz |
| 10 | Morogoro | 89 | 023 | 0738267155 | morogoro@meteo.go.tz |
| 11 | Moshi | 353 | 027 | 0733889535 | moshi@meteo.go.tz |
| 12 | Babati-Manyara | 356 | - | 0736674360 | babati@meteo.go.tz |
| 13 | Kilwa Masoko | 20 | 023 | 0737087279/ 0784822841 | kilwa.masoko@meteo.go.tz |
| 14 | Mtwara | 17 | 023 | 0737210057/ 0694944123 | mtwara@meteo.go.tz |
| 15 | Musoma | 89 | 028 | 0754361155 | musoma@meteo.go.tz |
| 16 | Mwanza | 701 | 028 | 0762605235 | mwz@meteo.go.tz |
| 17 | Same | 36 | 027 | 0737475027 | same@meteo.go.tz |
| 18 | Shinyanga | 248 | 028 | | shinyanga@meteo.go.tz |
| 19 | Singida | 563 | 026 | 0755215778 | singida@meteo.go.tz |
| 20 | Songea | 73 | 025 | 0735398364 | songea@meteo.go.tz |
| 21 | Sumbawanga | 306 | 025 | 0753577583 | sumbawanga@meteo.go.tz |
| 22 | Tabora | 40 | 026 | 0737285663 | tabora@meteo.go.tz |
| 23 | Tanga | 977 | 027 | 0734031910 | tanga@meteo.go.tz |
| 24 | Pemba | 169 | 024 | 0777461440 | pemba@meteo.go.tz |
| 25 | Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa Kigoma | 301 | 028 | 0754452444 | nmtc@meteo.go.tz |

## Vituo vya hali ya hewa - kilimo

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hombolo-Dodoma | 203 | 027 | 0769896071 | hombolo@meteo.go.tz |
| 2 | Igeri - Njombe | 299 | - | 0733339502/ 0754208845 | igeri@meteo.go.tz |
| 3 | Ilonga - Kilosa | 75 | - | 0717612286 | ilonga@meteo.go.tz |
| 4 | Kibaha - Pwani | 30460 | 023 | 0736438750/ 0764438750 | kibaha@meteo.go.tz |
| 5 | Kizimbani - Zanzibar | 30031 | 023 | 0773648485 | kizimbani@meteo.go.tz |
| 6 | Lyamungu - Moshi | 159 | - | 0765989826 | lyamungu@meteo.go.tz |
| 7 | Mlingano -Tanga | 3004 | - | 0734031910 | mlingano@meteo.go.tz |
| 8 | Naliendele - Mtwara | 89 | 023 | 0737210057/ 0694944123 | naliendele@meteo.go.tz |
| 9 | Tumbi -Tabora | 509 | 023 | 0737285663 | tumbi@meteo.go.tz |
| 10 | Ukiriguru -Mwanza | 306 | - | 0762605235 | ukiriguru@meteo.go.tz |
| 11 | Uyole -Mbeya | 1433 | - | 0755853588 | uyole@meteo.go.tz |
| 12 | Mbimba -Mbozi | 11 | | | mbimba.mbozi@meteo.go.tz |
| 13 | Matangatuani - Pemba | 169 | 024 | 0777461440 | matangatuani@meteo.go.tz |

## Vituo vya hali ya hewa shughuli za kwenye maji (Marine)

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam Port Met | 3056 | 022 | | marine@meteo.go.tz |
| 2. | Kigoma Port Met | 278 | 028 | 0746531918/ 0737131906 | kigoma.marine@meteo.go.tz |
| 3. | Itungi-Kyela Port Met | 344 | 025 | | kyela.marine@meteo.go.tz |
| 4. | Pemba Port Met | 169 | 024 | 077461440 | pemba.marine@meteo.go.tz |
| 5. | Tanga Port Met | 977 | 027 | 0734031910 | tanga.marine@meteo.go.tz |
| 6. | Zanzibar Port Met | 340 | 024 | 0773648485 | zanzibar.marine@meteo.go.tz |
| 7. | Mwanza Port Met | 701 | 028 | 0762605235 | Mwanza.marine@meteo.go.tz |
| 8. | Karema Port Met | | | 0746855884 | |




**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Godfrey Kazinja

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline_TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.